

Disciples' Network

Luka 10:19

Jarida la kila Mwezi

UTANGULIZI

Tunakusalimu katika jina la YESU Kristo!

Tunamshukuru Mungu kwa kutuwezesha kuumaliza mwezi Mei (mwezi wa uinjilisti) kwa ushindi.

Ndani ya mwezi Mei, Mungu ametuwezesha kuwa na matukio mengi ya baraka katika majiji ya Dar es Salaam, Mwanza na Arusha. Baadhi ya matukio ni Mafunzo ya Utumishi yaliyoambatana na ubatizo jijini Arusha, fellowship za kati kati ya wiki na kila Jumamosi, mikesha ya kila Ijumaa kwa njia ya mtandao, mafundisho ya neno la MUNCU, maombi kwa njia ya Google Meet pamoja na huduma ya ushauri na maombezi.

Vilevile tumefanikiwa kuwa na semina ya vijana wa kike na kiume wasio kwenye ndoa (Singles in the wait) iliyohudhuriwa na vijana 1,680 (1,560 walishiriki kwa njia ya mtandao)



Disciples' Network

Katika semina hii vijana walijifunza masomo muhimu ya maandalizi ya ndoa na afya ya uzazi. Pia yalifanyika maombezi maalumu kwa vijana wote. Shukrani za pekee kwa wazungumzaji wote walio-jitolea kuwafundisha vijana masuala muhimu na nyeti yahusuyo hatma zao.

Ndani ya mwezi wa tano vilevile, tumeweza kuanzisha makundi maalumu ya wanawake walio kwenye ndoa, wanaume walio kwenye ndoa, vijana wa kiume na wajane. Awali lilikuwepo kundi na vijana wa kike tu. Makundi haya yanarahisisha utoaji wa huduma wa haraka kwa walengwa.

Shuhuda nyingi zimeripotiwa wakati wa ibada na kwenye makundi yetu ya huduma ya WhatsApp, na tunamshukuru Mungu kwa neema yake na uamini-fu wake kwetu. (Wakolosai 3: 17)

MAHUDHURIO

Idadi ya waliohudhuria ibada zetu mwezi Mei 2023 ni kama ifuatavyo:-

	Arusha	DSM	Mwanza
Wanawake	38	562	205
Wanaume	6	228	23
Watoto		68	
Mtandaoni		2,916	

Jumla ya waliofikiwa na ibada zetu kwa mwezi mei ni 4,046.

MATUKIO

(a) Ubatizo



Katika mwezi Mei, tumefanikiwa kuwabatiza watu 25 Arusha tulibatiza watu 11 (wanawake 10 na mwanaume 1), Mwanza watu 7 (wote wanawake) na kayenze watu 7 (wanawake 5 wanaume 2). (Matendo ya Mitume 2:41)

(b) Kuhamasisha Jamii kujikinga dhidi ya magonjwa ya mlipuko

Disciples Community kwa kushirikiana na serikali ya mtaa pamoja na kata ya Kawe, tumefanikiwa kuhamasisha jamii juu ya Kuhamasisha jamii kujikinga na magonjwa ya mlipuko.



MAADHIMISHO YA SIKU YA MAMA DUNIANI

Mnamo tarehe 13 Mei, tulipata wasaa mzuri wa kuonesha upendo kwa akina mama wenyewe uhitaji na wajane, kwa kuwapatia chakula na fedha kidogo za kujikimu, katika kuadhimisha siku ya Mama Duniani. (Yakobo 1:27)



MAMBO YAJAYO


Maandiko yanatuambia tuombe bila kukoma, 1 Thes. 5:16-18, tunaomba maombi yako kwa ajili ya yafuatayo:

- Ombea utekelezaji wa mipango na mikakati ya kumzalia Bwana Yesu matunda zaidi, ndani ya mwezi wa sita amba ni mwezi wa Pente-koste.
- Ombea semina ya vijana wadogo (teenagers), Jumamosi ya mwisho wa mwezi Juni, 2023.
- Ombea wagonjwa wote na wenyewe shida mbalimbali.
- Ombea ubatizo, Jumapili ya mwisho wa mwezi Juni.
- Ombea huduma ya Disciples Network na watenda kazi wote.



RATIBA ZA IBADA

Tunakualika kushirikiana katika kueneza Injili ya YESU Kristo. Vile vile tunakualika wewe na familia yako, ndugu, jamaa na marafiki kujeungu nasi kwenye ibada zetu ambazo hufanyika Dar es Salaam, Mwanza na Arusha.



MAHALI	SIKU	TUKIO	MUDA
Dar-es-Salaam	Jumatano Ijumaa Jumamosi	Maombi Mkesha Online Fellowship	11:30 Jioni 05:00 Usiku 07:00 Mchana
Mwanza	Jumanne Jumatano na Alhamisi	Maombi kwa kupitia Google Meet	04:00 Usiku
	Jumamosi	Fellowship	07:00 Mchana
Arusha	Jumanne Jumamosi ya mwisho wa Mwezi	Fellowship Fellowship	11:00 Jioni 07:00 Mchana

MAWASILIANO

Dar es salaam
+255 755 999 198 / +255 687 222 197

Mwanza
+255 753 853 493

Arusha
+255 717 108 306

- DISCIPLES' NETWORK**
- DNETWORK**
- DISCIPLESNETWORK**
- DISCIPLES' NETWORK**